



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA MBUNGE JIMBO LA
KONDE, PEMBA

Dodoma, 2 Agosti, 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), yenye Kumb. Na. CCM/T.40/8vol.I/72 ya tarehe 2 Agosti, 2021, ikitoa taarifa kuwa Mbunge Mteule wa Jimbo la Konde Ndugu Sheha Mpemba Faki aliandika barua kwa chama hicho, kukitaarifu kuwa hayupo tayari kuwawakilisha wananchi wa Jimbo la Konde katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kutokana na changamoto za kifamilia.

Kutokana na hatua hiyo, Tume inatoa taarifa kwa umma kuwa Jimbo la Konde lipo wazi, na taratibu za kujaza nafasi hiyo zitatangazwa hivi karibuni. Tume imefanya hivyo kwa kuwa ilikuwa bado haijamjulisha Mh. Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kuhusu kukamilika kwa uchaguzi katika Jimbo la Konde na kuchaguliwa kwa Mbunge huyo Mteule. Aidha, Tume ilikuwa haijamtangaza kwenye Gazeti la Serikali kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 81(c)(iii) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343.

Ikumbukwe kuwa awali Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge katika Jimbo la Konde Mkoa wa Kaskazini Pemba - Zanzibar. Nafasi hiyo ilitokana na kufariki kwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo tajwa Mheshimiwa Khatibu Saidi Haji kupitia chama cha Alliance for Change and Transparency (ACT -WAZALENDO).

Kutokana na taarifa hiyo kutolewa na Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa kifungu cha 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliitisha uchaguzi uliofanyika tarehe 18 Julai, 2021.

Imetolewa na



Dkt. Wilson Mahera Charles
MKURUGENZI WA UCHAGUZI